



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



Julai 13, 2023

TAARIFA KWA UMMA

PONGEZI KWA SHULE ZOTE ZA SEKONDARI ZA WILAYA YA LUDEWA KWA KUONGEZA UFAULU KATIKA MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA

Kufuatia Baraza la Mitihani la Tanzania kutangaza matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita leo Julai 13, 2023 kwa mwaka 2023, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Ndugu Sunday Deogratias ametuma salamu za pongezi kwa shule tatu zilizokuwa na Watahiniwa wa kidato cha sita mwaka 2022/2023 kwa kupata ufaulu wa juu na hivyo kuondoa kabisa daraja sifuri.

Pongezi hizo amezituma kwa Mkuu wa shule ya Sekondari Chief Kidulile ambapo Shule hiyo imepiga hatua kubwa kwa kupata ufaulu wa asilimia mia moja. Ufaulu kwa shule tatu za Sekondari Chief Kidulile, Mundindi na Ulayasi ni kama ifuatavyo:-

SHULE YA SEKONDARI CHIEF KIDULILE

MWAKA 2023						MWAKA 2022				
SEX	I	II	III	IV	0	I	II	III	IV	0
F	30	23	5	0	0	2	11	15	0	0
M	32	23	2	0	0	4	28	26	1	0
T	62	46	7	0	0	6	39	41	1	0

SHULE YA SEKONDARI MUNDINDI

MWAKA 2023						MWAKA 2022				
SEX	I	II	III	IV	0	I	II	III	IV	0
F	12	41	2	0	0	7	26	11	0	0
M	14	53	3	0	0	13	43	10	0	0
T	26	94	5	0	0	20	69	21	0	0

SHULE YA SEKONDARI ULAYASI

MWAKA 2023						MWAKA 2022				
SEX	I	II	III	IV	0	I	II	III	IV	0
F	3	28	23	0	0	2	22	14	0	0
M	13	22	15	0	0	10	29	14	3	0
T	16	50	38	0	0	12	51	28	3	0

Kutokana na matokeo hayo kuwa mazuri ukilinganisha na mwaka 2022, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias amewapongeza Walimu wa shule zote tatu kwa kazi nzuri. Aidha amewaasa Walimu kuendelea kutekeleza majukumu kwa bidii ili kuongeza kasi ya ufulu kwenye Shule zote zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Chrispin B. Kalinga

**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini (W)
LUDEWA.**

Ludewa ya Utalii, Uchumi wa Chuma na Makaa ya Mawe kwa Maendeleo Yetu.